

## **HATUA ZA KUOTESHA UYOGA MAMAMA (oyster mushroom) KWA KUTUMIA KIMENG'ENYWA CHA MAJANI (JUNCAO).**

1. Kusanya majani makuvu (Juncao,mgomba, mpunga, ngano,nk)
2. Katakata majani vipande vidogovidogo ukubwa wa sentimita 1 hadi 2.
3. Pima uzito wa majani yako.
4. Pima majivu, au chokaa asilimia moja ya uzito wa majani yako.
5. Loweka majani kwenye maji kwa mda wa dakika tano, baada ya kuloweka weka majani yako kwenye trubai au nylon safi.
6. Changanya majani na asilimia moja ya majivu au chokaa.
7. Kusanya pamoja majani kutengeneza kichuguu, funika vizuri wa mda wa siku1, hadi siku7.
8. Jaza majani kwenye viriba (mifuko) kwa kushindilia vizuri na kwa umakini usitoboe mifuko, mifuko inayotoboka izibwe vizuri na gundi ya karatasi.
9. Takasa mashamba yako kwa mvuke kwa kutumia pipa lenye maji, kwa mda masaa4 ya moto mkali usiopungua pungua.
- 10.Hamisha mashamba katika chumba cha kupandia, yaweke kwenye trubai au nylon iliyosafishwa vizuri na Dettol (viua wadudu). Acha yapoe kwa mda wa saa12 hadi24.
- 11.Panda mbegu kwa kusambaza kijiko kimoja kimoja kwa kila upande mmoja wa shamba. Chupa moja ya mbegu ipande mashamba 10 hadi12.
- 12.Weka mashamba yako katika chumba chenye mwanga hafifu, mizizi ya uyoga hukua vizuri katika mwanga hafifu. Mizizi hukua na kusambaa shamba lote kwa kipindi cha wiki2 hadi 4.
- 13.Baada ya mizizi kutambaa shamba lote, ongeza mwanga ndani ya banda na fungua mashamba yako pande moja au mbili.
- 14.Nyunyizia maji mara moja kwa siku sehemu za shamba zilizo wazi kwa kutumia pampu ya mkono au mgongoni, uyoga utaanza kutokeza siku ya5 hadi ya7.